Kitini cha makala ya amri ya kuzuiliwa

YALIYOMO

Mateso ya nyumbani ni nini? 1

Amri ya kuzuiliwa ni nini? 1

Ninawezaje kumuombea mtu amri ya kuzuiliwa? 2

Kuhudhulia mahakamani 2

Inakuaje unapofika mahakamani? 3

Mahakamani inakuwaje? 3

Inakuwaje kama amri ya kuzuiliwa imekubarika? 4

Baadaye inakuwaje? 5

Inakuwaje endapo mtuhumiwa amekiuka amri? 5

Nini kuhusu amri ya mahakama ya familia? 6

Inakuwaje endapo ninahitaji kubadirisha amri ya kuzuiliwa? 6

Wapi unaweza kupata msaada? 7

Hati ya kukataa 8

Mateso ya nyumbani ni nini?

Mateso ya nyumbani hutokea katika sehemu zote za jamii yetu na katika tamaduni zote. Mateso ya nyumbani ni matumizi mabaya ya nguvu kati ya watu wanaoishi pamoja, au baada ya kutengana kutokana na uwanja mpana wa kitabia. Haya huweza kuwa mateso ya kimuili na kijinsia, kunyimwa matumizi au kuwekewa mipaka ya kiuchumi. Hizi tabia zote hazikubariki katika jamii yetu, na baadhi yake zinakwenda kinyume cha sheria.

Lengo la polisi ya Australia ya Kusini ni kulinda na kuzidisha usalama kwa wanaoonewa majumbani. Hii amri ya kuzuiliwa huweza kukulinda wewe pamoja na familia yako. Makala haya yanakueleza kinachotokea utakapolipoti polisi na kuomba amri ya kuzuiliwa. Ni matumaini yetu kwamba makala haya yatajibu maswali yako, na yatakusaidia kuchukua uwamuzi kuhusu jambo la kufanya.

Amri ya kuzuiliwa ni nini?

Amri ya kuzuiliwa ni amri ya mahakama inayomzuia mtu (mtuhumiwa) kuendeleza tabia ya matusi, unyanyasaji, vitisho au mateso kwako wewe (mlalamikaji). Mtuhumiwa anaweza kuamriwa kutofanya vitu kadhaa kama vile kutokuja nyumbani kwako, kutokwenda shule ya mtoto wako,kutokufuatilia, au kukuchunguza, kutokutumia ujumbe. Amri hiyo imefanywa hasa kwa ajili yako na hali yako.

Ni kosa la jinai kwa mtuhumiwa kufanya jambo moja kati ya hayo anayozuiliwa kufanya na amri hiyo. Hii inaitwa kukiuka amri. Ni lazima uyitaarifu polisi endapo mtu atafanya moja ya haya mambo.

Ninawezaje kumuombea mtu amri ya kuzuiliwa?

Kwa kawaida kwenda polisi ni njia rahisi ya kuweza kumuombea mtu amri ya kuzuiliwa.

Ni vizuri sana kwenda umejiandaa . Utakapokwenda uende na ushahidi wowote au taarifa unayofikiria kwamba itakusaidia kuthibitisha unachosema. Hii inaweza kuwa ni pamomja na:

- Maandishi yoyote ambayo unaweza kuwa umeandika kuhusu mambo yaliyofanywa na mtuhumiwa ikiwa ni pamoja na taarifa kuhusu ni wakati gani na ni wapi jambo lililofanyika.
- Picha yoyote au ushahidi mwingine ambao unaonyesha uharibifu uliofanywa nyumbani kwako.
- Nakala yoyote ya amri ya kuzuiliwa iliyotolewa na mahakama ya familia kuhusu watoto wako.

Ni lazima uiambie polisi kama unafikiria kwamba mtuhumiwa ana bunduki. Endapo amri ya kuzuiliwa itatolewa, mahakama itaamuru pia hiyo bunduki ikamatwe kwa mda wote wa amri hiyo. Taarifa ya kiapo, inayoitwa hati ya kiapo itachukuliwa kutoka kwako. Hii itataja istoria ya hali yako na ni msingi wa maombi yako ya amri ya kuzuiliwa. Unapokula kiapo, unaiambia mahakama kwamba kila kitu unachosema ni ukweli mtupu. Ni kosa la jinai kusema uongo katika hati ya kiapo. Hati yako ya kiapo itapelekwa polisi katika Kitengo cha makosa ya uhalifu ambako polisi mwendesha mashtaka atafanya uchunguzi na kuona kama kuna jambo la msingi la kuyiomba mahakama ikupatie amri ya kuzuiliwa. Endapo itakuwa hivo, polisi itakuwakilisha mahakamani. Kwa kawaida utalazimika kwenda mahakamani, lakini polisi atazungumza kwa niaba yako.

Katika maeneo ya mjini:
- Utaambiwa ni lini utakwenda mahakama ya hakimu mkazi.

Katika maeneo ya vijijini:
- Polisi, Kitengo cha makosa ya uharifu atakutaarifu endapo utahitaji kuhudhulia mahakamani.

Kuhudhulia mahakamani

Hakikisha kuwa unafika mahakamani mda ulioambiwa na ofisa wa polisi, kama unaona kwamba utachelewa au hutaweza kufika, piga simu polisi au mahakamani mapema iwezekanavyo na utoe sababu.

Utakapofika mahakamani, muulize mfanyakazi wa mapokezi ni chumba gani cha mahakama unatakiwa kwenda.

Inakuaje unapofika mahakamani?

Kama unahudhuria mahakama ya mjini, utakutana na ofisa wa polisi ambaye atakuelekeza. Kama unahudhuria mahakama ya kijijini, ofisa wa polisi muendesha mashtaka atakueleza. Endapo utakuwa hujasoma na kutoa hati ya kiapo, watakufanyia mpango ufanye hivo mbele ofisa wa polisi anayerushusiwa au mtu mwenye mamlaka kisheria. Kumbuka kwamba ni kosa la jinai kutoa hati ya kiapo ambayo ina taarifa za uongo.

Kwa vile hati ya kiapo yako itatumika mahakamani kama ushahidi, unaweza usihitaji kujieleza mahakamani kwa mazungumzo. Lakini, ingawa unaweza usihitaji kutoa maelezo, ni lazima uwepo mahakamani.

Utaombwa kusubiri nje ya chumba cha mahakama mpaka hapo hakimu atakapokuwa tayari kusikiliza maombi yako. Ofisa wa mahakama atakuingiza kwa wakati mwafaka.

Mahakamani inakuwaje?

Mtu ambaye utakuwa umemuombea amri ya kuzuiliwa hatakuwa mahakamani kufuatilia maombi yako. Endapo atakuwepo kwa sababu nyingine yoyote, na hujisikii kuwa na usalama, umtaarifu ofisa wa polisi au mfanyakazi wa mahakama.

Wakati hakimu yuko tayari kusikiliza maombi yako, utaombwa kuingia katika chumba cya mahakama na kukaa kwenye viti vya nyuma. Utakaposikia jina la mtu uliyemshtaki, kazi itakua inakaribia kuanza. Hii ni urasmi wa mahakama na vinamaanisha kwamba hakimu yuko tayari kusikiliza mashtaka yako.

Utaendelea kukaa. Hutakiwi kufanya kitu chochote kwa wakati huu, labda kama hakimu, mfanyakizi wa mahakama au ofisa wa polisi atakuomba kufanya hivo.

Endapo hakimu atahitaji maelezo kuhusu jambo fulani, anaweza kukuomba kwenda katika sehemu ya washahidi ili uulizwe swali. Mara nyingine wanaweza kukuuliza maswali ukiwa bado umekaa huko nyuma ya mahakama, na unaweza kujibia huko. Ofisa wa polisi huweza pia kukuuliza maswali kama atahitaji maelezo zaidi kuhusu jambo fulani. Unapashwa kusikiliza swali kwa makini na kujibu kwa uhakika na kwa ukweli.

Baada ya hakimu kuchukua uwamuzi wake, atakujulisha endapo amri ya kuzuiliwa imekubalika.

Utapashwa kusikiliza anachokuambia hakimu baada ya kusoma maombi yako. Kama kuna kitu ambacho huelewi, unaweza ukamuuliza ofisa wa polisi baada ya kikao cha mahakama, na ofisa huyo atakueleza kilichotokea na atajibu maswali yoyote ambayo unaweza kuwa nayo.

Inakuwaje kama amri ya kuzuiliwa imekubarika?

Mahakama itatoa amri siku hiyo, lakini, ni muhimu uelewe kwamba hiyo **amri haiwezi kuanza kufanya kazi mpaka hapo polisi yenyewe** (mfuatiliaji wa amri) **itakapotoa nakala yake kwa mtuhumiwa**. Kama itawezekana, usimuambie mutuhumiwa kwamba polisi inatarajia kumpatia amri ya kuzuiliwa kwa vile anaweza akasababisha polisi isifanye kazi yake kwa urahisi.

Polisi itakuambia ni lini nakala ya amri ya kuzuiliwa imetolewa, lakini endapo utakuwa na mashaka unaweza ukauliza kwenye kituo cha polisi kilichopo karibu na wewe wakati wowote.

Utapata **nakala tatu** za amri ya kuzuiliwa ya maombi yako kwa njia ya posta au kutoka polisi siku chache baada ya kuhudhulia mahakama, au kutoka polisi siku chache baada ya kuhudhulia mahakamani. Ni vizuri kutunza nakala moja sehemu yenye usalama, na nyingine ukawa unatembea nayo (kwa mfano katika begi au ndani ya gari), na nakala ya tatu unaweza kumpatia mtu mwinyine ambaye anaweza kuihitaji (kwa mfano shule anakosoma mtoto wako).

Soma nakala yako kwa makini ili uweze kujua ni jambo gani mtuhumiwa (mshitakiwa) analoweza kufanya na asiloweza kufanya kwa; namna hiyo, unajua endapo mtu mwingine amefanya kitu ambacho ni kinyume na kile alichozuiliwa kufanya, katika hali hii unaweza kuijulisha polisi.

Mara nyingine amri imetolewa kwa mda fulani, kwa mfano, mwaka mmoja au myaka miwili. Kama amri hayionyeshi mda, maana yake ni kwamba itaendelea.

Baadaye inakuwaje?

Amri ya kuzuiliwa pia inaonyesha tarehe ya kwenda mahakamani endapo mtuhumiwa hakubaliani na uamzi uliotolewa katika amri hiyo.
Polisi itajaribu kuchunguza jambo ambalo hakubaliani nalo, na itakujulisha endapo kuna mabadiliko katika amri hiyo. **Hulazimiki kwenda mahakamani kwenye hii tarehe**. Kama mtuhumiwa ataendelea kutokubaliana na amri baada ya kikao cha mahakama, basi kutakuwa na kesi mahakamani baadaye.

Polisi itakuambia kama utakwenda mahakamani. Endapo utakwenda itakuambia ni lini na ni wapi utakwenda. **Endapo utakwenda mahakamani, wakati huu utatoa ushahidi na utakaa sehemu ya washahidi.** Mtuhumiwa (mshitakiwa) naye atakuwa mahakamani ili aweze kusikiliza, kwa hiyo kama hutajisikia salama, utaiambia polisi na hatua zitachukuliwa ili wajalibu kukufanya ujisikie salama.

Ni muhimu kukumbuka kwamba amri ya kuzuiliwa itaendelea kufanya kazi mpaka mwisho wa mashtaka kusikilizwa. Mahakama inaweza kuthibitisha kwamba amri inaendelea. Endapo itaamuliwa hivo, amri itaendelea kukulinda mpaka hapo mda wake utakapokwisha, au kubadilishwa na mahakama.

Inakuwaje endapo mtuhumiwa amekiuka amri?

Endapo mtuhumiwa atavunja kipengele kimojawapo cha amri, hii inaitwa kikiuka amri. Hili ni kosa la jinai.

Ni lazima ufanye kila linalowezekana kutokwenda kinyume na amri au kumfanya mtu mwingine kufanya hivo. Kwa mfano kama mtuhumiwa haruhusiwi kuwasiliana na wewe, basi na wewe usiende kumtembelea au isimpigie simu. Ukifanya hivo utakuwa unavunja sheria na unaweza ukahukumiwa kwa kosa hilo.

Endapo uvunjaji wa amri ya kuzuiliwa utafanywa na mtuhumiwa au ukiona kwamba uko hatarini, mara moja piga simu namba 131 444 (au 000 wakati wa dharura) na wana usalama watakuja kukusaidia.

Endapo utafikiria kwamba ukiukwaji wa amri umetokea lakini humo hartarini (kwa mfano kama mtuhumiwa amekwenda shuleni kumuona mtoto kinyume na alivyoambiwa), unatakiwa kuripoti hali hii kwenye kituo cha polisi kilichopo karibu na wewe, ili polisi iweze kuchunguza.

Ukumbuke kwamba amri ya kuzuiliwa yako itafanya kazi kikamilifu kama utaruhusu hivo; kwa hivyo unapashwa kuripoti kila kitu.

Nini kuhusu amri ya mahakama ya familia?

Kama watoto wamehusishwa, **itakuwa lazima upate ushauri wa kisheria** ambao utakusaidia kuamua kama utaomba amri ya Mahakama ya familia. Ni muhimu kukumbuka kwamba uamuzi wa mahakama ya familia **unaweza kubadili uamuzi ambao ulikuwa umetolewa katika amri ya kuzuiliwa.** Polisi inaweza kukueleza hayo.

Inakuwaje endapo ninahitaji kubadirisha amri ya kuzuiliwa?

Kama hali imebadirika na unataka kubadiri moja ya vipengele vya uamuzi katika amri ya kuzuiliwa au kuifuta, unaweza ukawasiliana na kitengo cha uchunguzi kwa watoto na familia au kituo cha polisi na kuwaambia ni kwa sababu gani unataka kubadirisha amri ya kuzuiliwa au kuyifuta.

Kikao kingine cha mahakama kitalazimika kupangwa ili mahakama isikiliza uamuzi wako, ndipo amri yoyote itaweza kubadilishwa au kufutwa. Ni lazima uelewe kwamba ni mahakama peke yake ambayo inaweza kubadilisha au kufuta amri. Wewe mwenyewe huna uwezo wa kubadilisha amri uliyoomba na mtu mwingine kukubari mabadiriko hayo.

Wewe na mtuhumiwa mtaelezwa wakati na tarehe ya kusikilizwa. Hapa utahitajika kuhudhuria mahakamani. Mara nyingine mtuhumiwa naye atalazimika kuhudhuria.

Polisi na mahakama hutambua kwamba mara nyingine hali hubadirika kuwa nzuri, na amri nayo inaweza ikabadirika pia. Lakini, polisi inapashwa kulidhika kwamba utaendelea kuwa salama na hukulazimishwa na mtu yeyote kubadiri mawazo, jambo ambalo linaweza kukuingiza wewe mwenyewe au familia yako katika matatizo makubwa.

Mara nyingine polisi haitakubari kukata rufaa na kukuwakilisha mahakamani kwa maombi ya kurekebisha au kufuta amri ya kuzuiliwa, kama inaamini kwamba uwamuzi huu utaongeza matatizo ambayo baadaye yatasababisha mateso kwako au familia yako nyumbani.

Wapi unaweza kupata msaada

Kwa hali ya dharura	000		
Kwa msaada wa polisi	131 444		
Polisi kitengo cha uchunguzi kwa watoto na familia			
Adelaide	8463 7090	Baada ya kazi	8346 7007
Elizabeth	8207 9353	Baada ya kazi	8207 9442
Holden Hill	8207 6034	Baada ya kazi	8207 6000
Port Adelaide	8207 6413	Baada ya kazi	8207 6444
South Coast	8392 9172	Baada ya kazi	8392 9000
Sturt	8207 4801	Baada ya kazi	8207 4700
Sehemu za vijijini, wasiliana na kituo cha polisi kilichopo karibu nawe.			

Kama umepata mateso ya nyumbani, na huwezi kuongea Kiingereza, na unahitaji msaada wa kuelewa hatua za kuomba amri ya kuzuiliwa, tafadhali uwasiliane na **mashirika ya kutoa huduma za misaada na makazi kwa wanawake wahamiaji** kwa kutumia namba ya simu: **83469417.**

Listi ya mashirika ambayo yanaweza kutoa msaada zaidi au kukuunga mkono, wewe kama mtu aliyepata mateso ya nyumbani,inapatikana kwenye kituo cha polisi kilichopo karibu na wewe.

Hati ya kukataa: Makala haya yameandaliwa kwa ari ya polisi ya Australia ya Kusini kwa ajili ya kuisaidia jamii. Makala haya yanatoa taarifa za kijumla kama muongozo kusaidia kuendeleza usalama na kupunguza uhalifu.

Ingawa makala haya yameandaliwa kwa uangalifu mkubwa, hakuna uhakika au uthibitisho kwamba yaliyozungumziwa katika makala haya yamefanyiwa utafiti. Hakuna utafiti uliofanywa kuhusu usahihi, usawa na utosherezaji wa taarifa au ushauri vilivyomo katika makala haya.

Hakuna uhakika au uthibitisho kwamba yaliyozungumziwa au yaliyolengwa katika makala haya yemefanyiwa utafiti kuhusu athari za taarifa au ushauri vilivyomo katika makala haya. Hakuna dhima au kuhusika vitakavyokubarika kwa makosa yoyote au ujumbe ulioachwa katika makala haya, au mtu yeyote kupoteza kitu kutokana na athari za kuamini sana taarifa zilizomo katika makala haya.

Wasomaji wanashauliwa kutafuta mawakili huru, pamoja na ushauri mwingine wa kitaalamu kutokana na hali ya kila mtu.

Hati ya kumiliki © 2005 ya serikali ya South Australia (Australia ya Kusini)
Makala haya ni mali ya Malkia na Serikali ya Austalia ya Kusini. Licha ya matumizi yaliyoruhusiwa na sheria ya mwaka 1968 ya hati ya kumiliki, hakuna sehemu yoyote ya makala haya ambayo inaruhusiwa kunakiliwa kwa njia nyingine yoyote ile bila ya ruhusa iliyotolewa kwa maandishi ya mwenye kumiliki makala haya. Maombi yanapashwa kutumwa kwa: South Australian Police, Box 1539, GPO, ADELAIDE, South Australia 5001.

Shukrani zimetolewa kwa TAFE SA Adelaide South, Elimu ya Sheria, kwa ushirikiano wao katika kutunga na kuandika taarifa zilizomo katika kitini hiki.

Kitini hiki kimetolewa kwa ushirikiano wa Kitengo cha Kupunguza uhalifu cha polisi ya Australia ya Kusini, na mratibu wa waathiriwa wa uhalifu, Kitengo cha Kuboresha Sheria, na Kitengo cha Sheria na Siasa cha Idara ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.